TANGAZO LA SERIKALI Na. 39 la Tarehe. 24/1/2025

SHERIA YA USIMAMIZI NA TOZO YA USHURU
(SURA. 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MAWILI YANAYOINGIZWA NCHINI NA WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA (TFS) KATIKA MRADI WA KUJENGA USTAHIMILIVU WA BIONUAI YA MISITU DHIDI YA MATISHIO YA MABADILIKO YA TABIA YA NCHI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Mawili yanayoingizwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Bionuai ya Misitu dhidi ya Matishio ya Mabadiliko ya Tabia ya Nchi ya mwaka 2024 itaanza kutumika kuanzia tarehe 14 Novemba, 2024

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na magari mawili yaliyoainishwa kwenye jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Bionuai ya Misitu dhidi ya Matishio ya Mabadiliko ya Tabia ya Nchi umesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu

mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika Ukomo tarehe 13, Machi, 2025

JEDWALI

*(Imetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| SN | Maelezo | Mwaka | Namba ya Injini | Idadi | Namba ya Chassis | Mahali |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser Hardtop 10 seater, 5 doors | 2024 | 1HZ-1078050 | 01 | JTEEB71J80F031313 | limeagizwa |
| 2 | Toyota Land Cruiser Hardtop 10 seater, 5 doors | 2024 | 1HZ-1078146 | 01 | JTEEB71J10F031329 | limeagizwa |

Dodoma
30 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*